Refugee
SELF-RELIANCE
Initiative

# ZANA YA KUPIMA UWEZO WA KUJITEGEMEA

## Toleo la 2.0:
### Viashiria vya kupima hatua za kuanza kujitegemea



## Shukrani

Zana ya Kupima Uwezo wa Kujitegemea (SRI) ni zana iliyoundwa kwa ushirikiano kati ya wanachama wa Refugee Self-Reliance Initiative (www.refugeeselfreliance.org), chini ya uongozi wa RefugePoint na Women's Refugee Commission. Waandalizi wakuu wa nakala ya rasimu walikuwa Kellie Leeson (mtalaamu, RSRI), Dale Buscher (Women's Refugee Commission) na Amy Slaughter (RefugePoint). Vyanzo vikuu vilivyochangia katika kuunda zana hii ni pamoja na Zana ya Kupima Kiwango cha Kujitegemea (Self-Reliance Measurement Tool) iliyoandaliwa na RefugePoint na Zana ya Well-Being and Adjustment Zana iliyoandaliwa na Women's Refugee Commission. Shukrani kuu kwa Dkt. Lindsay Stark na Ilana Seff kwa uongozi wao wa kitaalamu na ushauri wao katika mchakato wote wa kuunda na kujaribu zana hii.

Tunatuma shukrani za kipekee kwa mashirika na wafanyakazi wa vituo vinne vya tathmini kwa maoni ya thamani waliyotupa, hasa Reilly Ross, Ahmad Hiyari (Danish Refugee Council/Jordan), Galo Quizanga Zambrano, Adriana Monar, Oswaldo Aguilar, Manuel Pozo (HIAS/Ecuador), Paul Karanja, Walter Gitau (RefugePoint/Kenya), Maria Angelica Montesinos na Alejandra Macias (Asylum Access/Mexico). Matoleo ya awali ya Zana ya Kupima Uwezo wa Kujitegemea yaliwasilishwa katika warsha ya 2017 ya Oxford Refugee Studies Centre iliyoitwa "Livelihoods, Self-Reliance, and the 'Refugee Entrepreneur': Rethinking Refugee Self-Reliance" na pia mkutano wa washikadau wa 2019 ulioitwa Refugee Self-Reliance Initiative ambao uliandaliwa mjini Amman, Yordani.

Mwishowe, tunawashukuru wachangiaji wengi walioachangia katika maandalizi ya zana hii kupitia mawasiliano ya kila mara, hasa: William Axinn (Chuo Kikuu cha Michigan), Ziad Ayoubi (UNHCR), Prem Bhandari (Chuo Kikuu cha Michigan), Stefanie Barratt (Samuel Hall), Theresa Beltramo (UNHCR), Christina Boehm (Danish Refugee Council), Jacob Bonyo (RefugePoint), Sasha Chanoff (RefugePoint), Frank Chege (Mercy Corps), Nell Compernolle (Chuo Kikuu cha Michigan), Jaime Costigan (International Rescue Committee), Khadra Elmi (Joint IDP Profiling Service), Christine Forster (Mercy Corps), Lori Fried (Trickle Up), Walter Gitau (RefugePoint), Alisha Guffey (Idara ya Serikali ya Marekani/PRM), Erica Harper (Taasisi ya West Asia-North Africa), Janet Heisey (Trickle Up), Alison Hemberger (Mercy Corps), Paul Karanja (RefugePoint), Patience Kiara (Regional Durable Solutions Secretariat), Shezane Kirubi (Regional Durable Solutions Secretariat), John Lakeman (Danish Refugee Council), George Lehner (RefugePoint), Nassim Majidi (Samuel Hall), Ned Meerdink (RefugePoint) Karene Melloul (Solutions Alliance), Sasha Muench (Mercy Corps), Elizabeth Mukami (International Rescue Committee), Sophia Mungai (Danish Refugee Council), Ly Nguyen (Ikea Foundation), Robert Nyambaka (UNHCR), Tendayi Nyanhete (Trickle Up), Rebecca Gathu Nyokabi (RefugePoint), Naohiko Omata (Refugee Studies Centre, University of Oxford), George Oduor (UNHCR), Katherine Perkins (US State Dept/PRM), Patrick Poulin (International Rescue Committee), Simar Singh (RefugePoint), Roger Swartz (RefugePoint), na Pauline Vidal (Samuel Hall).

Kwa maswali na maelezo zaidi, tafadhali wasiliana nasi ukitumia barua pepe betterlivesnow@refugepoint.org.

Zana ya Viashiria vya Kupima Kiwango cha Kujitegemea cha Wakimbizi (SRI) imeidhinishwa na RefugePoint na Women's Refugee Commission chini ya Leseni ya Kimataifa ya Creative Commons Attribution-NonCommercial 4.0 International License.

# VIASHIRIA VYA KUPIMA KIWANGO CHA KUJITEGEMEA (SRI) ni Nini?

...ni zana inayotumiwa kupima maendeleo ya familia za wakimbizi katika harakati za kujitegemea kwa kurejelea kipindi fulani cha muda.

Viashiria vya Kupima Kiwango cha Kujitegemea cha Wakimbizi (SRI) ni zana inayotumiwa kupima maendeleo wa familia za wakimbizi katika harakati za kujitegemea kwa kurejelea kipindi fulani cha muda. Kimsingi, SRI imenuiwa kuwasaidia watekelezaji mikakati kuunda na kutoa huduma zinazowafaa zaidi wakimbizi katika nchi ambazo wameomba makao. Pia inaweza kusaidia katika kulenga wakimbizi ili kuwapa usaidizi, huku ukiangazia mapengo katika huduma zinazotolewa na kusaidia katika kubaini sehemu kuu za kuzingatiwa zaidi katika ufadhili. SRI ni zana iliyoandaliwa kupitia mchakato wa kujumuisha wadau. Mchakato huu ulijumuisha washiriki zaidi ya 25 wanaoshughulikia masuala ya wakimbizi, wakiwemo Mashirika Yasiyo ya Serikali (NGO), UNHCR, mashirika ya utafiti, wakfu kadhaa na mashirika ya serikali. SRI iliandaliwa ili kujaza pengo kuu katika kuwezesha fursa za wakimbizi kujitegemea kupitia kutoa tathmini ya kina ya kiwango cha juu, inayosimamiwa kuhusu mabadiliko makuu ya familia za wakimbizi. Zana hii inatarajiwa kubadilika na kuboreshwa kwa kuwa inaendelea kusaidia wakimbizi duniani kote kujenga maisha yao.

Hati hii imegawanywa katika sehemu tatu - ufafanuzi wa SRI na matumizi yake, katika sehemu ya pili tunawasilisha zana hii kwenye ukurasa 6-17, na hatimaye kupata mwongozo wa kutoa alama kwenye ukurasa wa 19.

1.




2.




3.



# MUHTASARI


Je, kusudi la Viashiria vya Kupima Kiwango cha Kujitegemea cha Wakimbizi (SRI) ni lipi? 3

Je, zana hii inatumiwa kwa njia gani? 5




# Je, kusudi la SRI ni lipi?

## Kuboresha Miradi ya Kuwasaidia Wakimbizi

SRI iliundwa ili kufuatilia maendeleo katika familia za wakimbizi na hatua zao katika harakati za kujitegemea. Iakini pia inaweza kutumiwa kutathmini uwezo wa kujitegemea kwa watu wengine waliotoroshwa makwao na wale wanaotoa makao.

Kwa hivyo, zana hii ina lengo la kusaidia katika kuunda na kutekeleza miradi kwa manufaa ya wakimbizi. Hili linatokea katika kiwango cha kila familia (kuboresha misaada kwa watu binafsi na kwa nyumba za wakimbizi na kiwango cha programu ili kuboresha na kutoa michango katika maandalizi ya miradi ifaayo. Zana hii inaweza kutumiwa katika kulenga nakuchunguza wateja wanaohitaji msaada na pia kufuatilia maendeleo yao katika kipindi fulani cha muda na ina uwezo wa kusaidia wateja ambao "wamehitimu" kutoka kupokea misaada wakati ambapo hawaihitaji tena.

SRI inaweza kusaidia katika aina zote za programu, iwe mikakati inalenga sekta fulani kama vile sekta ya afya au njia za familia kujikimu au huduma nyingine pana zaidi. Kama kuwa SRI inalenga kufuatilia au kwa kuzingatia ukosefu wa muda, inaweza kusaidia mashirika kuzipa huduma zao vipaumbele na watu ambao wameelekezwa kwao katika vitengo ambavyo maendeleo yanatokea polepole au hayapo.

## Ufuatiliaji na Tathmini

Mbali na kufuatilia matokeo ya familia za wakimbizi, SRI inaweza kusaidia katika kiwango cha ufuatiliaji wa miradi ili kutambua vyema zaidi matokeo ya jumla ya misaada na huduma zote zinazotolewa kwa familia za wapokeaji misaada. Ikiwa asilimia kubwa ya mahitaji ya wateja na shirika moja, SRI inaonyesha ufanisi wa programu hizo, hali ambayo huenda ikachangia katika kufanya maamuzi kuhusu usimamizi wa misaada.

Ikiwa kwa hali nyingine misaada inatolewa kupitia watoa huduma wengine kadhaa, zana hii huenda ikaashiria ufanisi wa kijumla wa watoa huduma hao. Hii inaweza kuchangia katika ushirikiano mkubwa baina ya watoa huduma husika.

SRI inaweza kuwasaidia wafadhili kubaini vyema zaidi ufanisi wa programu zilizopo au mkusanyiko wa programu ambazo wanazifadhili. Pia inaweza kubaini mapengo yanayohitaji rasilimali zaidi.

## Utafiti

Data iliyokusanywa kutokana na matumizi ya SRI inaweza kutumiwa kusaidia kubaini mbinu na kulinganisha vigezo mbalimbali baina ya makundi fulani ya watu, maeneo na kuonyesha uhusiano wa ufanisi wa aina mbalimbali ya miradi inayochangia katika kukuza uwezo wa kujitegemea.

**Kujitegemea:** Uwezo wa kiuchumi na kijamii wa mtu binafsi, familia au hata jamii kukidhi mahitaji ya msingi katika njia ifaayo.

## Je, SRI inalenga nani ?

Kimsingi, SRI iliundwa ili kutumiwa kwa wakimbizi wanaoishi mijini na wasioishi katika kambi za wakimbizi katika nchi au maeneo ambayo wameomba makazi baada ya kutoroka nchi zao kwa mara ya kwanza. Japo haijatathminiwa, SRI pia inaweza kuwa muhimu watu wengine ambao wamepoteza au wamefukuzwa kutokwa kwa makao yao, wakiwemo wakimbizi wa ndani ya nchi, wakimbizi wanaoishi katika kambi au wanaoishi sehemu za mashambani, wakimbizi wa kiuchumi na hata watu ambao wamo katika hatari ya kuwa wakimbizi katika nchi husika. Pia inaweza kutumiwa kwa wakimbizi ambao wamepewa makao au ambao wamerejeshwa kwao.

Kwa kuwa zana hii inalenga kufuatilia maendeleo katika kipindi fulani cha muda, SRI haijalenga kutumiwa kwa wakimbizi ambao wamo katika mpito (kwa mfano wakimbizi wanaopitia kwa muda mfupi wakiwa njiani kuelekea sehemu nyingine). Kimsingi, zana hii inalengwa kutumiwa kwa wakimbizi ambao kwa kiwango fulani ni thabiti kulingana na eneo lao, ikiwa wakimbizi hao ni wakazi halali au si wakazi halali. Inaeleweka kwamba SRI haiwezi kufaa katika matumizi ya kila siku katika kila hali na kwamba kunaweza kuwa na hali ambapo kupima maendeleo katika kiwango cha familia hakufai.

## Je, SRI inaweza kutumiwa na nani?

SRI "zana wazi" na inaweza kutumiwa na mtu yeyote. SRI imetolewa chini ya leseni ya Creative Commons, ambayo inaruhusu mtu yeyote kuitumia zana hii kwa madhumuni yasiyo ya kibiashara na inahitaji watumiaji kutambua chanzo cha zana hii. Watoa huduma wanaosaidia wakimbizi ambao hawaishi katika kambi na aina yoyote ya msaada (kwa mfano njia za kujikimu, pesa taslimu, chakula, matibabu na afya, ulinzi wa watoto, usimamizi wa kesi fulani ya wakimbizi, n.k.) wanatarajiwa kunufaika na SRI. Watoa huduma hawa wanaweza kujumuisha Mashirika Yasiyo ya Serikali (NGO), mashirika yanayojumuisha idara za serikali na mashirika ya serikali. Katika mashirika haya, inatarajiwa kwamba wasimamizi wa wakimbizi fulani wasimamizi wa miradi au wataalamu wa Ufuatiliaji na Tathmini wanaweza kupewa jukumu la kuwapa wateja SRI ili kutathmini hali ya wateja wao.

Inatarajiwa kwamba mashirika yanayotumia SRI watathmini wateja wao kwa kutumia vigezo vyote vya tathmini, licha ya lengo mahususi ya mpango wao au sekta wanayolenga. Katika njia hii, SRI inaweza kuhimiza uhusiano wa karibu miongoni mwa huduma za misaada kwa binadamu, maendeleo na huduma za serikali ili kuhakikisha misaada kamilifu kwa familia za wakimbizi. Hata mashirika yanayotoa msaada inayolenga sekta mahususi (kwa mfano, misaada inayolenga ulinzi wa watoto) wanaweza kupata ukamilifu wa hali ya familia kutokana na matokeo yanayotolewa na SRI ili kuunda huduma zao kwa njia inayofaa zaidi na maswali hayahitaji maarifa ya kiufundi yanayohusisha sekta husika ili kuyajibu. Kama ilivyofafanuliwa hapo juu, wafadhili na watafiti huenda pia wakanufaika kutokana na matumizi ya SRI.

Ingawa SRI inaweza kutumiwa na mtu yeyote, watumiaji wanahimizwa kukagua kwa makini Mwongozo wa Matumizi na kuingia katika mkataba wa ushirikiano na RSRI ili kupokea mafundisho yoyote yaliyopo ili waweze kunufaika kutokana na marekebisho ya mara kwa mara kadri yanavyotolewa. Pia ni muhimu kwa kuwa itawawezesha kushiriki katika matumizi ya zana katika jamii na hata kuhimiza ujifunzaji wa kimataifa kupitia ukusanyaji na uchanganuzi wa data.

## Je, kuna Mwongozo wa Matumizi wa SRI?

Ndiyo, tafadhali omba mwongozo wa matumizi unaopatikana kwenye tovuti ya Refugee Self-Reliance Initiative (refugeeselfreliance.org). Maelezo ya kijumla ya jinsi ya kutumia SRI yametolewa.

## Mifumo ya Kukusanya Data ya SRI

Kwa sasa, SRI inaweza kutathminiwa kwa kutumia mifumo ya kukusanya data ya CommCare na Kobo. RSRI itaendelea kuwazia kupanua SRI ili kujumuisha mifumo ya kukusanya data baadaye.

# Je, zana hii inatumiwa kwa njia gani?

## Mara za Kutumia Zana

Inakusudiwa kwamba SRI itapewa wateja sawa baada ya kila miezi 3 au 6 kwa kipindi cha muda wanaopokea huduma za usaidizi au wanaopokea misaada. Ikiwa "watahitimu" kutoka hali ya kupokea misaada, inapendekezwa ufuatiliaji uendelee katika familia hii kwa kipindi fulani cha muda baada ya kipindi cha kupokea msaada kukamilika. Hali hii itasaidia katika kuhakikisha kuna uendelevu katika kujitegemea tukizingatia hali tatanishi ya wakimbizi.

## Tathmini ikilinganishwa na Hojaji

SRI **haijaundwa** kama hojaji ya kusoma swali moja kwa moja na kurekodi tu majibu ya wateja. Bali, hii ni zana ya kumsaidia anayefanya tathmini katika kufanya tathmini faafu ya hali ya familia kwa kutegemea vitengo vinavyotathminiwa. Anayefanya tathmini atatumia mkusanyiko wa majadiliano na wateja, kuchunguza kwa kuangalia moja kwa moja (kwa mfano, kutembelea nyumba husika), maarifa kuhusu hali za eneo ambapo familia inaishi na maelezo mengine yoyote aliyo nayo kuhusu hali za familia anayofanya tathmini, ili kuafikia tathmini kamilifu kuhusu familia hiyo.

Ieleweke kwamba anayefanya tathmini kuwa na mapendeleo kuhusu suala fulani inaweza kuathiri matumizi ya zana hii. Mwongozo wa Matumizi unafafanua vipengele vya kutathmini katika kila kitengo ili kupunguza mapendeleo pamoja na kutoa mafunzo na mbinu za usimamizi ili kufanikisha ukubalifu wa matokeo ya SRI. Ufahamu wa muktadha wa eneo familia inaishi utasaidia katika kupunguza mapendeleo ya anayefanya tathmini.

## Wanaotathminiwa

Kwa ajili ya kufuatilia data inayopatikana kuna haja ya kutambua "Anayetathminiwa Ili Kuwakilisha Familia" kwa kila familia, lakini mtu huyo sio lazima awe mkubwa wa familia kama inavyotambulika kitamaduni. Ikiwezekana, hatua zinahitaji kuchukuliwa ili kujumuisha maoni ya wanafamilia wote. Changamoto inayoweza kutokea ni katika kupima kiwango cha familia ili kutoa alama moja inayolengwa kuashiria maoni kamilifu ya wanafamilia wote. Uzoefu unaweza kutofautiana kutoka mtu mmoja hadi mwingine, hasa kulingana na umri, jinsia, afya na tofauti zingine. Pamoja na SRI, anayefanya tathmini huenda angependa kutumia zana za utafiti zinazotoa ufafanuzi zaidi ili kutathmini tofauti za hali miongoni mwa wanafamilia.

## Kutoa Alama

Chaguo za majibu za SRI haziwezi kushughulikia tofauti zote katika hali fulani ya familia. Anayefanya tathmini sharti achague chaguo ambalo linakaribiana zaidi na hali za familia zinazotathminiwa. Hesabu ya alama imeratibiwa ili kufanyika kiotomatiki kwenye matoleo ya kidijitali ya zana. Kiolezo cha Muundo wa Excel kilicho na fomula kitatolewa kwa wale ambao hawatumii toleo la kidijitali la zana. Alama katika kila kitengo zinaweza kusaidia katika kuwaelekeza wakimbizi kupata usaidizi wa huduma wanazohitaji au kuboresha mwitikio wa wadau kulingana na sekta husika. Alama za jumla za familia huashiria kiwango jumuishi cha familia cha kujitegemea. Mashirika huenda yangependa kuweka vipimo vya chini na juu zaidi vya alama ili kuibua matukio fulanvile kuingizwa katika mradi au kuondolewa kwenye mradi, kama vile kuingizwa katika mradi au kuondolewa kwenye mradi.

## Kutojitosheleza

SRI haijaundwa kutosheleza chanzo cha maelezo ambayo mashirika yanahitaji kwa ajili ya kuandaa na kutekeleza miradi yao. Watoa huduma huenda wangependa kukusanya maelezo zaidi ili kuelewa mahitaji na changamoto zinazoikumba kila familia na wanafamilia wake. SRI inaweza kusaidia kutimiza lengo hili ikitumiwa pamoja na zana zingine za kufanyia ufuatiliaji.

## Urahisi

Mwisho, ni kwamba imepunguzwa hadi vitengo vichache ambavyo ni muhimu katika kutathmini kiwango cha kujitegemea. Zana hii imeundwa ili kutumika kwa urahisi na kuzingatia muda wa familia za wakimbizi. Lengo la SRI ni kutoa kiashiria kikamilifu cha kiwango cha juu kinachoweza kutegemewa kuhusu familia za wakimbizi kujitegemea kutokana na uzoefu wao na mabadiliko ambayo yametokea muda unavyosonga.

# VIASHIRIA VYA KUPIMA KIWANGO CHA KUJITEGEMEA CHA WAKIMBIZI


**SEHEMU YA 1:** Maelezo ya Kibaiografia 7

**SEHEMU YA 2:** Vitengo Vinavyotathminiwa 8

**SEHEMU YA 3:** Maswali Wazi 15

**SEHEMU YA 4:** Tathmini ya Mhojaji 16






# **Sehemu ya 1:** Maelezo ya Kibaiografia

## Maelozo ya Mhojaji

| | | |
|---|---|---|
| Jina la Mhojaji | | |
| Tarehe ya Tathmini | | Jinsia Kike ☐ Kiume ☐ Nyingine ☐ |
| Wakala | | |

## Maelezo ya Mteja*

| | | | |
|---|---|---|---|
| Maelezo ya Mtathminiwa Mkuu | | | |
| Uraia | | | |
| Nambari ya Familia au Utambulisho | | Jinsia Kike ☐ Kiume ☐ Nyingine ☐ | |
| Kama haya ni matembezi baada ya matembezi mengine ya awali: Jina la anayehojiwa ikiwa ni mpya awali hapatikani | | | |
| Lugha msingi inayozungumzwa nyumbani (zisizidi lugha 2) | 1. | 2. | |
| Hati alizonazo mwakilishi wa familia (tia alama kwenye hati zote ?alizonazo) | ☐ Nambari ya Usajili ya UNHCR | ☐ ya Nchi Mkimbizi Anaishi | ☐ Nyingine (tafadhali bainisha) |
| Tafadhali onyesha hati inayohitajika ili kuishi kihalali kwenye nchi unayoishi (tia alama kwenye moja) | ☐ Nambari ya Usajili ya UNHCR | ☐ ya Nchi Mkimbizi Anaishi | ☐ Nyingine (tafadhali bainisha) |
| | Je, wanafamilia wote wa nyumba hii wamesajiliwa kwa kutumia hati hii?<br>Wote ☐ Wengine ☐ Hamna Yeyot ☐ | | |
| Lugha inayotumiwa kuzungumza na mhojiwa wakati wa mahojiano ya kutathmini kwa kutumia SRI | 1. | 2. | |
| Idadi ya wanafamilia (Orodhesha umri na jinsia ya kila mmojaaliye katika familiamajina hayahitajiki) | | | |
| Dadi ya | Watoto (0-17) | Watu Wazima (18-59) | Wazee (60+) |
| Uwiano wa Utegemeaji | | | |
| Tarehe (ya karibu zaidi) ya kuwasili katika Nchi ya Makazi | | | |
| Anwani ya mahali unapoishi sasa | | | Umeishi hapa kwa muda gani? |
| Njia ya mawasiliano ambayo ungependa tutumie kuwasiliana nawe (moja tu inahitajika, lakini tafadhali hakikisha kuna angalau mbili) | Nambari ya au za Simu/ WhatsApp Unazotumia Sana | Maelezo ya Ziada ya Mawasiliano (nambari nyingine ya simu au WhatsApp) | |

* Maelezo ya kibaiografia hayataonyesha jina katika hifadhi jumla ili yalinde faragha na siri ya maelezo ya mteja



# KITENGO CHA 1: NYUMBA

## KITENGO CHA 1A: UTOSHELEVU WA NYUMBA

**Lengo:** Kubainisha aina ya nyumba ya familia na utoshelevu wake (ukubwa na ubora).

### Swali linaloongoza kitengo:

Je, unaweza kueleza hali ya sasa ya nyumba yako?

1. Hakuna nyumba
2. Nyumba ya muda (kibanda, kioski, gari)/ Wanadamu hawafai kuishi katika nyumba
3. Tunaishi kwa marafiki, familia, jamii, makazi ya kundi la kidini au makao ya dharura kwa kipindi cha muda mfupi
4. Nyumba au nyumba ya ghorofa ya kukodisha, haitoshi
5. Nyumba au nyumba ya ghorofa ya kukodisha, haitoshi

Ikiwa familia inaishi katika ghorofa au nyumba, uliza mhojiwa ikiwa anahisi au hahisi nyumba inatosha.

**Jumuisha maoni yoyote muhimu hapa (pamoja na maelezo yoyote yanayofaa kuhusu ukubwa na ubora wa nyumba):**

## KITENGO CHA 1B: KUKODISHA

**Lengo:** Kubaini uwezo wa familia kupata nyumba wanayoweza kulipia.

### Swali linaloongoza kitengo:

Je, katika miezi 3 ambayo imepita, ni miezi ngapi **hujaweza** kulipa kodi?

1. Mara 2-3
2. Mara 1
3. Hamna Yeyote
4. Sijakodisha

Swali hili linalenga uwezo wa familia kulipa kodi, licha ya ikiwa pesa zipo au hazipo.

**Jumuisha maoni yoyote muhimu hapa:**

# KITENGO CHA 2: CHAKULA

**Lengo:** Kubaini ikiwa familia inakula chakula cha kutosha na kifaacho.

## Swali linaloongoza kitengo:

Je, unaweza kueleza hali ya chakula na milo ya familia jana?

1. Familia hawakula jana
2. Familia waliweza kula lakini, sio milo kamili
3. Familia iliweza kula mlo 1 kamili
4. Familia iliweza kula milo kamili mara 2-3

**Jumuisha maoni yoyote muhimu hapa (pamoja na chakula cha jana ulaji haukuwa kawaida ya upatikanaji wa chakula wa kaya):**

- Ikiwa huna hakika kama chakula wanachokula kinajumuisha mlo kamili, muulize mhojiwa kama wanafamilia walihisi kuwa chakula kinatosha
- Toa alama ya familia kulingana na mwanafamilia mwenye alama ya chini zaidi.

# KITENGO CHA 3: ELIMU

**Lengo:** Kubaini ikiwa watoto wenye umri wa kwenda shule wapo shuleni.

Alama ya Elimu hurejelea masomo ya rasmi ya shule ya msingi na upili na hulenga kupata maelezo ikiwa watoto wanaenda shuleni, licha ya hali ya vikwazo vinavyoathiri mahudhurio ya shule. Mhojaji anahitaji kuuliza maswali zaidi ili kujua sababu za kutohudhuria shule au kutohudhuria kwa ukawaida.

## Swali linaloongoza kitengo:

Je, katika miezi 3 iliyopita, watoto wenye umri wa kwenda shule katika familia yako wamekuwa wakienda shuleni?

0. Hakuna watoto wenye umri wa kwenda shule kwa nyumba hii
1. Hamna yeyote aliye shuleni
2. Wengine wako shule
3. Watoto Wote wako shuleni

- "Walio shuleni" inafasiliwa kuwa zaidi ya asilimia 50 ya wakati shule zimefunguliwa
- Umri wa kwenda shule unapaswa kufasiliwa kulingana na kanuni na sheria za nchini.

**Jumuisha maelezo yoyote muhimu hapa, hasa maelezo yoyote kuhusu kwa nini watoto hawaendi shuleni (wanafanya kazi, vikwazo vya karo, usalama, n.k.):**

# KITENGO CHA 4: MATIBABU

**Lengo:** Kubaini ikiwa familia inaweza kupata matibabu ikiwa wanahitaji kutibiwa.

## Swali linaloongoza kitengo:

Je, katika miezi 3 iliyopita, familia yao imeweza kupata matibabu waliyokuwa wanahitaji?

0. Familia haijahitaji matibabu katika miezi 3 iliyopita
1. Hatukupata matibabu tuliyohitaji
2. Tulipokea matibabu fulani tuliyohitaji
3. Tulipokea mahitaji yote tuliyohitaji

Alama ya matibabu inajumuisha matibabu ya msingi na maalum, ikiwa ni pamoja na hali kali na za kudumu za wanafamilia wote.

**Jumuisha maoni yoyote muhimu hapa:**

# KITENGO CHA 5: HALI YA AFYA

**Lengo:** Kubaini uwepo wa hali ya kiafya (kiakili au kimwili) ambayo inaweza kuathiri vibaya uwezo wa familia kuweza kujikimu

## Swali linaloongoza kitengo:

Je, kuna mtu yeyote katika familia yako kwa sasa ambaye ana hali ya kimwili na kisaikolojia ambayo inaathiri shughuli za kuzalisha mapato?

1. Mtu au watu wazima katika familia wana hali ya kiafya inayowazuia kupata ajira ya watu wazima.
2. Mtu au watu wanaonitegemea wana hali ya kiafya ambayo inawazuia kabisa kupata ajira ya watu wazima
3. Hakuna wowote kati ya waliotajwa

Ikiwa chaguo mbili au tatu zinalingana na hali za familia, chagua alama ya chini zaidi inayotumika.

**Jumuisha maoni yoyote muhimu hapa:**

# KITENGO CHA 6: USALAMA

**Lengo:** Kubaini ikiwa ufahamu wa familia wa usalama unazuia uwezo wa kutafuta fursa mbalimbali.

## Swali linaloongoza kitengo:

Je, kwa sasa familia yako inahisi kuwa salama ili kutafuta fursa za kijamii, kiuchumi na kielimu ambazo wangependa?

1. Hawahisi salama ili kutafuta fursa zozote
2. Wanahisi salama kutafuta baadhi ya fursa
3. Wanahisi salama kutafuta fursa zote

- Weka alama ya mwanafamilia mwenye alama ya chini zaidi.

**Jumuisha maoni yoyote muhimu hapa:**

# KITENGO CHA 7: AJIRA

**Lengo:** Kubaini ikiwa familia inashiriki katika shughuli za kuzalisha mapato.

Alama za Ajira sharti zizingatie shughuli zozote za kuzalisha mapato: kujiajiri, ujira, ajira rasmi au isiyo rasmi, ajira ya muda, biashara ndogo, n.k. Toa alama ya juu zaidi inapatikana kwa mtu mzima yeyote wa familia (kwa mfano, ikiwa mtu mzima ameajiriwa wakati wote na mwingine ameajiriwa kwa kipindi cha muda, wape alama ajira ya kudumu). Ajira ya kudumu au ya muda inaweza kujumuisha kazi tofauti tofauti.

## Swali linaloongoza kitengo:

Je, unaweza kufafanua shughuli za kuchuma mapato ambazo wanafamilia wanashiriki, wameshiriki katika miezi 3 iliyopita?

1. Hakuna ajira
2. Ajira ya muda, isiyo ya kila siku, inayotegemea kipindi fulani
3. Ajira ya mara kwa mara ya kipindi fulani* (ikiwemo kujiajiri)
4. Ajira ya kudumu (ikiwemo kujiajiri), bila hati halali zinazohitajika.
5. Ajira ya kudumu (ikiwemo kujiajiri), ukiwa na hati halali, ikiwezekana

- Ikiwa chagio moja au kadhaa zinalingana na hali ya familia, chagua alama ya juu zaidi inayotumika.
- "Ajira ya muda" inafasiliwa kuwa chini ya saa 35 kwa wiki. Ajira ya kudumu ni ya zaidi ya saa 35 kwa siku.

**Jumuisha maoni muhimu hapa hasa ikiwa kuna hali ambapo kuna ajira ya watoto:**

# KITENGO CHA 8: RASILIMALI ZA KIFEDHA

**Lengo:** Kubaini vyanzo vya kukidhi mahitaji ya msingi ya familia.

Familia zinaweza kutumia vyanzo mbalimbali kushughulikia mahitaji yao ya kimsingi, kulipa kodi, msaada wa kifedha, ujira na mapato kutoka shughuli ya kuzalisha mapato, michango kutoka kwa watu wengine, miongoni mwa vyanzo vingine.

## Swali linaloongoza kitengo:

### Je, katika miezi 3 iliyopita, familia yako inajikimu vipi kutimiza mahitaji yake ya kila siku? [chaguo nyingi iwezekanavyo]:

1. Misaada (kwa mfano shirika la misaada, shirika la kidini au serikali
2. Kuomba pesa au kuomba chakula
3. Kuuza mali ya familia
4. Akiba uliyoweka hapo awali
5. Malipo/pesa/ michango kutoka kwa marafiki na jamaa
6. Kazi (kazi rasmi au isiyo rasmi),biashara ndogo ndogo, kazi za mikono, huduma, n.k.)

**Jumuisha maoni yoyote muhimu hapa:**

- Uliza kuhusu kila kipengele kilicho kwenye orodha
- Neno 'msaada' linarejelea msaada au ufadhili rasmi (pesa taslimu au bidhaa) unaotolewa na shirika, taasisi ya kidini, serikali au kundi lingine rasmi; chakula au pesa taslimu zinazotolewa na jamaa au marafiki wa karibu zinapaswa kuainishwa kama 'msaada'.

# KITENGO CHA 9: MISAADA

**Lengo:** Kubaini ikiwa familia inategemea misaada kushughulikia mahitaji ya Kimsingi

## Swali linaloongoza kitengo:

### Je, umetegemea misaada ili kutimiza mahitaji ya msingi katika miezi 3 iliyopita? [chaguo nyingi iwezekanavyo]:

0. Hakuna msaada
1. Chakula
2. Bili za Nyumba/Kodi ya Nyumba
3. Matibabu
4. Elimu (ya msingi na ya upili)
5. Nyingine (sharti ujumuishe maelezo)

**Jumuisha maoni yoyote muhimu hapa:**

- Uliza kuhusu kila kipengele kilicho kwenye orodha.
- Tazama ufafanuzi wa 'Msaada' hapo juu.

# KITENGO CHA 10: DENI

**Lengo:** Kubaini ikiwa familia imepata deni ili kutimiza mahitaji ya kimsingi ya familia.

## Swali linaloongoza kitengo:

Je, kwa sasa una deni lolote (bila kuzingatia udogo wake) la mahitaji yafuatayo yoyote? [chagua nyingi iwezekanavyo]:

0. Hakuna deni
1. Chakula
2. Bili za Nyumba/Kodi ya Nyumba
3. Matibabu
4. Elimu (ya msingi na upili)
5. Usafiri
6. Uwekezaji (sharti ujumuishe maelezo)

**Jumuisha maoni yoyote muhimu hapa:**

- Uliza kuhusu kila kipengele kwenye orodha
- Uwekezaji' unarejelea mkopo uliochukuliwa ili kuboresha kiwango cha maisha ya mtu kwa muda mrefu ujao, km. kuwekeza katika biashara, elimu ya juu, nyumba au gari nk.

# KITENGO CHA 11: AKIBA

**Lengo:** Kubaini ikiwa familia ina akiba yoyote kwa sasa.

## Swali linaloongoza kitengo:

Je, kwa sasa una pesa zozote ambazo umeweka kama akiba au umehifadhi mali ambayo unaweza kuuza ikihitajika?

1. La, sina akiba au mali yoyote ninayoweza kuuza
2. Ndiyo, lakini haitatosha kushughulikia mahitaji ya mwezi mmoja (mahitaji ya msingi)
3. Ndiyo, inaweza kushughulikia mahitaji ya mwezi mmoja (mahitaji ya msingi)
4. Ndiyo, inaweza kushughulikia mahitaji ya mwezi mmoja (mahitaji ya msingi) pamoja na kununua mali au kuwekeza tena katika biashara yangu au kudumu katika hali yoyote ya kiafya ya wastani inapotokea

**Jumuisha maoni yoyote muhimu hapa:**

# KITENGO CHA 12: MTAJI WA KIJAMI

## KITENGO CHA 12A: MTAJI WA KIFEDHA WA KIJAMII

**Lengo:** Kubaini mitandao ya kifedha inayopatikana kwa wanafamilia.

### Swali linaloongoza kitengo:

Je, ikiwa mtu yeyote katika familia yako atapatwa na dharura mnajua watu wanaoweza kuwakopesha pesa kushughulikia gharama zinazohusiana na hali hiyo?

1. Anajua hakuna yeyote anayeweza
2. Anajua mtu au ana jamii inayoweza kuwakopesha pesa

Jibu la mwanafamilia mwenye alama ya juu Zaidi.

**Jumuisha maoni yoyote muhimu hapa:**

## KITENGO CHA 12B: MTAJI WA UHUSIANO WA KIJAMII

**Lengo:** Kubaini mitandao na mahusiano yanayoweza kupatikana kwa familia.

### Uliza maswali mawili:

Je, kuna watu ambao wewe au wanafamilia wako huuliza ushauri na maelezo?

Je, kuna watu ambao wewe au wanafamilia wako huuliza ushauri na maelezo?

0. Hakuna
1. Wanafamilia huomba watu wengine ushauri au maelezo PEKEEE/PEKEE
2. Watu huomba wanafamilia ushauri au maelezo PEKEE
3. Zote 1 na 2

Kwa 'watu' tunamaanisha marafiki, familia, majirani nk. lakini sio taasisi au mashirika

**Jumuisha maoni yoyote muhimu hapa:**

## **Sehemu ya 3:** Maswali Wazi



1. Je, una maoni yoyote kutuuliza?

2. Kuna jambo lolote ambalo lingekusaidia wewe na familia yako kuweza kujitegemea?

## **Sehemu ya 4:** Tathmini ya Mhojaji



### Sehemu ya 4a:

Je, kuna masuala yoyote yaliyoibuka
hapa ambayo hayakushughulikiwa na vitengo hivi?

### Sehemu ya 4b:

Andika maelezo ya mtu yeyote unayeelekeza kwa misaada kwa madhumuni ya ufuatiliaji wa siku za baadaye:

## Maelezo:

# MWONGOZA WA KUTOA ALAMA

Mwongoza wa kutoa alama 19



# Mwongoza wa kutoa alama

| a | b | c | d | e | f | g | h | i | j | k | l | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kitengo | | Nakili majibu kutoka zana | Maagizo | Weka alama | Maagizo | Thamani | Maagizo | Alama ya jumla ya kitengo | | | | |
| Nyumba | 1a | | Kipengele cha # | | ----> | =E2 | ----> | | | | | |
| Kodi ya Nyumba | 1b | Je, alama kutoka zana ni 4? Ikiwa ndiyo, ruka kitengo kilichosalia | Kipengele cha # | | Jibu la '1' = Alama 1<br>'2' = 3<br>'3' = 5 | =Ubadilishaji wa jibu | ----> | | | | | |
| Chakula | 2 | | Kipengele cha # | | Jibu la '1 au 2' = Alama 1<br>'3' = 3<br>'4' = 5 | =Ubadilishaji wa jibu | Tumia katika L16 | | | | | |
| Elimu | 3 | Je, alama inatoka zana ya 0? Ikiwa ndiyo, ruka kitengo kilichosalia | Kipengele cha # | | Jibu la '1' = Alama 1<br>'2' = 3<br>'3' = 5 | =Ubadilishaji wa jibu | ----> | | | | | |
| Matibabu | 4 | Je, alama inatoka zana ya 0? Ikiwa ndiyo, ruka kitengo kilichosalia | Kipengele cha # | | Jibu la '1' = Alama 1<br>'2' = 3<br>'3' = 5 | =Ubadilishaji wa jibu | ----> | | | | | |
| Hali ya Afya | 5 | | Kipengele cha # | | ----> | =E6 | Tumia katika L16 | | | | | |
| Usalama | 6 | | Kipengele cha # | | Jibu la '1' = Alama 1<br>'2' = 3<br>'3' = 5 | =Ubadilishaji wa jibu | ----> | | | | | |
| Ajira | 7 | | Kipengele cha # | | ----> | =E8 | ----> | | | | | |
| Rasilimali za kifedha | 8 | | - IKIWA '6' haijachaguliwa, basi alama ni '1'<br>- IKIWA '6' imejachaguliwa NA chaguo lingine limechaguliwa, basi alama ni '3'<br>- IKIWA '6' ni chaguo la pekee lililochaguliwa, basi alama ni '5' | | ----> | =E9 | ----> | | | | | |
| Usaidizi | 9 | | Idadi ya vipengele | | Vipengele 3 na 4 = 1<br>Vipengele 2 = 2<br>Kipengele 1 = 3<br>Vipengele 0 = 5 | =Ubadilishaji wa jibu | Tumia katika L16 | | | | | |
| Deni | 10 | | Idadi ya vipengele (bila kujumuisha chaguo la 6) | | Vipengele 4 na 5 = 1<br>Vipengele 2 na 3 = 2<br>Kipengele 1 = 3<br>Vipengele 0 = 5 | =Ubadilishaji wa jibu | ----> | | | | | |
| Akiba | 11 | | Kipengele cha # | | Jibu la '1' = Alama 1<br>'2' = 3<br>'3' = 4<br>'4' = 5 | =Ubadilishaji wa jibu | ----> | | | | | |
| Rasilimali ya kijamii | 12a | | Kipengele cha # | | Jibu la '1' = Alama 1<br>'2'=5 | =Ubadilishaji wa jibu | Wastani wa 12a na 12b | | | | | |
| | 12b | | Kipengele cha # | | Jibu la '0' = Alama 1<br>'1' = 3<br>'2' = 3<br>'3' = 5 | =Ubadilishaji wa jibu | | | | | | Alama ya Jumla ya SRI: |
| | | | | | | Iadi jumla ya alama/ idadi ya vitengo vilivyowekwa alama: | | | - (5-alama ya 2)*0.15<br>- (3-alama ya 5)*0.1<br>- (5-alama ya 9)*0.2 | | Simba upya <1 = 1<br>Simba upya <5 = 5 | |

Maelezo:

## Maelezo:

Refugee
SELF-RELIANCE
Initiative